

# Barua kutoka Taizé

n° 270 Toleo Maalum SW

Tulipoamua, na wale wenye wajibu wa utume kwa vijana Chile, kuwa mkutano wa pili wa Kimataifa wa Amerika ya Kusini kufanyika Santiago kuanzia Disemba 8-12, 2010, hatukuwa na wazo kuwa 2010 utakuwa mwaka ambao, kwa watu wa Chile, majaribu yatalingana na furaha. Kwa kuandaa mkutano wa vijana mwaka wote huu wote uliwawezesha baadhi ya mabruda kushiriki haya yote.

Wakati huohuo ambapo watu wa Chile pamoja na nchi nyingine za Amerika ya kusini , wakisherekea miaka mia mbili ya kuzaliwa kwa jamhuri, ghasia ardhini na majini zilizosababisha maumivu kwao.

Tetemeko la ardhi mwezi Februari liliathiri walio maskini kuliko. Lakini ukarimu mwingi uliotoka ndani ya mshikamano na mioyo ya wananchi ulionyesha kwa kiasi gani watu wa Chile ni familia moja, waliongana katika tabu. Vijana wengi wa Chile walwasaidia wale waliopoteza nyumba na kazi. Walitoa muda na nguvu kujenga mediasaguas, nyumba ndogo ambazo zilitumika kama makazi ya muda.

Katika mwaka huo, wakazi wa mwanzo wa Chile, haswa watu wa Mapuche, walieleza maumivu na matakwa yao kwa kufanya mgomo mrefu wa kula.

Baadaye kidogo, sura za wachimba madini therathini na tatu wakiletwa juu aridhini mwa nchi baada ya ajali mgodini zilileta furaha kwa nchi yote na duniani kwa ujumla.

Mwanzoni wa mwezi Disemba, mkutano wa kimataifa uliwawezesha vijana, siyo tu kutoka Chile bali kutoka barani kote, kushirikishana furaha, maumivu na changamoto na hivyo kufanya kazi pamoja kujenga dunia yenye utu. Turifurahi kuwakaribisha vijana kutoka Haiti katika mkutano huu. Uwepo wao ulitukumbusha udhuni kubwa iliyosababishwa na tetemeko la ardhi la Januari 2010 nchini mwao. Vidonda vyao vingali vibichi. Kama hali ya kisiasa na kijamii kwenye nchi zitaruhusu, kati ya mkutano wa Santiago na mkutano wa Ulaya Rotterdam (mwishoni Disemba 2010), tutakwenda Haiti, safari ambayo itatupa njia ya kuonyesha mshikamano wa vijana kutoka mabara yote vile vile kuvutiwa: imani huwaweka watu imara katikati ya matatizo.

Tutaendelea kuomba nao katika mwaka wote ujao:

Mungu tegemeo letu, tunakukabidhi watu wa Haiti. Tumefadhahiswa kwa maumivu yasiyo na mfano kwa wasio na hatia, tunakuomba kufungua mioyo ya wote waletao misaada muhimu. Tunafahamu imani ya kina waliyonayo watu wa Haiti. Wasaidie wote wanaoumia; watie nguvu wote waliokatiswa tamaa; wafariji wote wenye majonzi; mwaga Roho yako ya faraja kwa watu hawa walio umizwa na wanao pendwa sana.

**BARUA 2011**

# Barua kutoka Chile

## FURAHA

Moyo wenye furaha, ambao ni maisha yako. Hacha nyuma majonzi![1] Huu wito wa kutoka kwa mtu mwenye imani ambaye aliishi kitambo kabla ya Kristu pia ni kwa ajili yetu leo.

Tunapitia majaribu na maumivu katika maisha yetu, wakati mwingine kwa kipindi kirefu. Lakini daima tunataka kujaribu na kutambua tena furaha ya kuishi.[2]

Furaha hii inatoka wapi?

Inaamshwa na mkutano usiotegemewa, kwa urafiki unaodumu, kwa uumbaji wa kisanii au pia kwa uzuri wa mazingira....

Upendo ulionyeshwa kwetu huiita ambayo taaratibu ujaza kina cha moyo.[3]

1 Angalia Nabii Sira bin'Shura 30:22-23. Mkristu wa karne ya pili aliyeitwa Hermas pia aliandika: "weka hali ya uchangamfu.... Wote wataishi kwa ajili ya Mungu ambaye huondoa huzuni wao, na wote kuwafanya wachangamfu."

2 Kinacholeta ukamilifu katika maisha ya binadamu siyo vitu vya ajabu, bali ni furaha tulivu ambayo hugusa kina cha moyo. Kutokamilika na hali ya vipande vipande ya kila maisha, pamoja maumivu, hakuondoki, hakuzimi utulivu.

3 Mwanatheolojia wa kanisa la mashariki Alexander Schmemann (1921-1983) aliandika katika kumbukumbu yake: "Furaha bila ya chochote cha msingi, bali furaha vilevile; furaha ya uwepo wa Mungu na uwazi wa moyo. Na kuushiriki huu mguso wa karibu, wa hii furaha (ambao hautoondolewa kwakuwa umekuwa ndani kabisa mwa moyo) utaongoza mawazo na mtazamo wa mtu maishani yote."

Nakisha tunaogozwa kufanya uamuzi, kuchagua furaha.

Wakati mwingine wale wanaopitia umasikini and ufukara wanaweza kupata furaha katika kuishi, furaha ambayo haikubali kukatishwa tamaa.[4]

Pia  Biblia utukumbusha tena na tena kuwa wenye furaha, inatuonyesha chanzo. Hii furaha haitegemei mapito tu; inatoka kwa Mungu: “Furahini katika kuunganika na Mungu daima. Nitasema tena: Furahini... Bwana yu karibu.”[5]

Kristu hakuja kuanzisha dini ambayo itakuwa kwenye mashindano na dini nyingine. Ndani yake, Mungu alishiriki hali yetu ili kila binadamu afahamu kuwa anapendwa kwa upendo wa milele na hivyo apate furaha katika muunganiko na Mungu. Tunapo mwamini macho yetu yanafunguliwa zaidi kwa yote yaliyo ya kibinadamu—upendo wa mama kwa mtoto wake, kujituma kwa wale wanaowatunza wagonjwa.... Katika matendo haya ya ukarimu Kristu yupo, wakati mwingine bila ya kutambulika.[6]

Kristu huleta mabadiliko mapya kwa wanadamu. Kwanza aliishi maisha haya mapya mwenyewe na aliangaika kubaki mwaminifu. Usiku kabla ya kukamatwa kwake alikata mkate akisema maneno haya ya ajabu: “Huu ni mwili wangu, ulitolewa kwa ajili yenu.”[7] Ndio, yeye ni “Neno lililofanywa mwili.”[8] Alibadili kifo chake kisicho na hatiak kuwa zawadi ya uhai wake. Kufuka kutoka wafu, aliweka pu mzi katika wafuasi wake kuwasilisha Roho mtakatifu, maisha yenyewe ya Mungu.[9]

Roho mtakatifu huweka furaha ya Kristu Mfufuka ndani mwetu. Siyo tu wakati mambo yanapokuwa marahisi. Tunapokabiliwa na changamoto, jitihada zinaweza kuamsha furaha. Na hata kipindi cha majaribu, inaweza kufukiwa kama kijinga cha moto chini ya majivu, bila kuzimika.[10] Kwa kutukuza, tunaacha iwepo ndani mwetu, na mara moja wakati uliopo unaangazwa.[11]

## HURUMA

Kuchagua furaha hakumaanishi kukimbia matatizo ya maisha. Badala yake, kunatuwezesha kukabiliana na uhalisia, na hata maumivu.

Kuchagua furaha hakuwezi kutenganishwa na mahitaji ya binadamu wengine. Kunatujaza na huruma isiyo na kikomo.

Kuonja furaha ya Mungu, japokuwa kwa vipindi, kunatufanya kuwa wanawake na wanaume wa muunganiko na Mungu. Ubinafsi kama njia ya furaha ni kiini macho.[12]

Kuwa mashahidi wa muunganiko na Mungu kunaitaji ujasiri wa kuogelea kinyume na mkondo. Roho mtakatifu atatupa mawazo tunayohitaji kutafuta njia za kubaki karibu na wale wenye maumivu, kuwasikiliza na kuathiriwa na hali za uzuni.[13]

4 Baada ya miaka mingi, bado ninawafikiria wale niliokutana nao Haiti nilipotembelea nchi na Bruda Roger. Katika nchi ile nzuri watu wanaishi kwa mashaka makubwa. Siwezi kusahau Wakina mama ambao mara nyingi asubuhi hawakujua kama watakuwa na chakula cha kutosha kuwalisha watoto wao katika hiyo siku. Na bado, kwa watu wengi wa Haiti, hata tetemeko kubwa la Januari 2010 halikuweza kuwafanya wapate mashaka katika imani yao kwa Mungu!

5 Wafilipi 4:4-5.

6 Angalia Matayo 25:35-40.

7 Luka 22:19.

8 Johane 1:14.

9 Johane 20:22.

10 Padri Basil Gondikakis, kiongozi wa monesteri kwenye Mlima Athos, alionyesha hili katika lugha ya kiimani iliyojaa ushairi: “Kwa mfano na msaada wa bikira Maria, kila roho yenye amani na uwazi, kwa mpango wa Mungu, waweza kuwa Mama wa Mungu kwa rehema, kupokea na kuzaa furaha ambayo inadili kifo.”

11 Kabla ya mateso yake, Yesu aliwaambia wafuasi wake: “Nanyi pia mna huzuni sasa, lakini nitawajieni tena, nanyi mtajaa furaha mioyoni mwenu, na furaha hiyo hakuna mtu atakayeiondoa kwenu” (Johane 16:22).

12 Mwanafalsafa wa Kiyahudi Martin Buber (1878-1965) aliandika: “Wewe wakutana nami kwa rehema—siyo kwa kukutafuta. Lakini kwa nikizungumzia neno la mwanzo, kusema Wewe, ni kitendo kwa utu wangu, kwa kweli ni kitendo cha utu wangu ... Ninakuwa mwenyewe kupitia uhusiano wangu kwa Wewe; jinsi ninavyokuwa Mimi, ninasema Wewe. Uhai wote wa kweli unakutana.”

13 Alberto Hurtado (1901-1952) ni mtakatifu kutoka Chile, aliyetangazwa na Pope Benedict XVI mwaka 2005. Padri huyu wa Kijesuit anatukuzwa katika nchi yake kwasababu ya maisha yake aliyoyatoa kwa maskini. Alianzisha “Nyumba za kristu” ambapo watu wasio na makazi, watoto, wanawake na wanaume walioko kwenye kipindi kigumu wanapewa malazi. Kauli mbiu ya maisha yake yote na matendo ilikuwa ni swali hili: Kristu angefanya nini kwenye nafasi yangu? Mwaka1947, aliandika kuhusu kuhusu wale waliokabithiwa kwake: “Kitu cha kwanza kufanya ni kuwapenda .... Kuwapenda sana kiasi ya kuwa siwezi kuvumilia maumivu yao .... Kazi yangu haiwezi kuishia kuwafariji kwa maneno mazuri na kuwaacha kwenye shida zao wakati ninakula kwa raha bila kukosa chochote. Maumivu yao lazima yaniuumize mimi .... Kuwapenda ili waweze kuishi, ili maisha ya binadamu yakue ndani mwao, ili akili zao zifunguke na wasibaki kando ya barabara.Kama tunawapenda, tutajua nini cha kuwafanyia. Je, Wataitikia? Ndio, kwa kiasi...na hakuna chochote kifanywacho kwa upendo kikapotea bure.”

Njia ya furaha, katika hatua za Yesu, ipo kwenye zawadi ya maisha yetu, kila siku. Kupita maisha tunayoishi, kwa urahisi mkubwa, twaweza kueleza Upendo wa Mungu.

Kama jumuiya zetu, parokia zetu na vikundi vya vijana vingeweza kuwa zaidi sehemu za wema wa moyo na imani ambapo tunakaribishana, ambapo tunatafuta maelewano na kusaidiana, sehemu ambazo tunawatambua wanyonge, wale ambao kwa kawaida hawako karibu nasi, mpaka wale ambao ni maskini kuliko sisi.

Ishara moja ya wakati wetu ni ukarimu mkubwa, watu wengi wamewasaidia wahanga wa maafa. Je yawezekanaje ukarimu huu kusukuma jamii zetu, hata katika maisha ya kila siku?[14]

Muhimu kama ulivyo msaada wa mali katika kipindi cha dharura, huo hautoshi. Kitu muhimu zaidi ni kurudisha haki kwa mafukara.[15]

Wakristu Amerika ya Kusini wanatukumbusha kuwa vita dhidi ya umasikini ni vita ya kutaka haki. Haki katika mahusiano ya kimataifa, na siyo misaada.[16]

Tunatakiwa kujifunza kuukabili uwoga. Tunafahamu wote juu ya matendo ya kujilinda ambayo yanahusisha kutaka kujiweka salama hata kwa gharama ya ustawi wa wengine. Na inaonekana kutajwa zaidi katika siku zetu, haswa hisia za uhaba zinavyoongezeka. Je, ni nini kinaweza kutuzuia kukubali uwoga? Je siyo kwa kuwafikia wengine, hata ambao wanonekana tishio?

14 Wakati wa ziara yake ya Uingeleza, Papa Benedict XVI alitoa wito huu: “Dunia imeshuhudia rasilimali nyingi ambazo serikali zimetumia kuokoa mashirika ya fedha ambayo yalionekakana ‘ni makubwa kuanguka’. Hakika maendeleo thabiti ya watu duniani yana umuhimu sawa: hili ni shirika, linalostahili umakini wa dunia, hili ndio kweli ‘kubwa kuanguka’.”

15 “Siyo mali zako ambazo unawagawia maskini, kwa urahisi unachofanya ni kwarudishia mali zao. Kwakuwa tu umejiwekea wewe tulivyopewa kutumia wote. Dunia ni ya wote na siyo matajiri peke yao, lakini ilibinafsishwa na wachache kwa gharama ya wengi ambao wanaishughulikia. Hivyo siyo kuwa unafanya ukarimu mkubwa bali unalipa deni tu.” (Ambrose wa Milan, karne ya nne)

16 Kwenye walaka wa mwisho wa mkutano uliofanyika Aparecida(Mei 2007), kanisa katoliki la Amerika ya Kusini, liliandika: “Kushughulikia uzuri wa pamoja inamanisha kuchochea taratibu zenye haki za kiuchumi, fedha na biashara za kimataifa. Ni muhimu kuwa mzigo w deni la nje uondolewe ili kukuza uwekezaji katika matumizi ya jamii na maendeleo. Taratibu za dunia zatakiwa kuzuia na kurekebisha mzunguko wa mitaji kwa ubashiri, kuchochea usawa wa biashara na kupunguza matendo ya kulinda masoko ya nchi tajiri, kuhakikisha bidhaa nzuri za rasilimali ghafi zizalishwazo katika nchi maskini na taratibu za haki katika kuvutia na kuzuia uwekezaji na huduma.

Uamiaji ni ishara nyingine ya nyakati zetu. Unaonekana kama hatari, lakini ni ”kiuhalisia upo na utaendelea kuathiri historia.”[17]

Ishara zaidi ya nyakati zetu ni kuongezeka kwa umasikini ndani ya nchi tajiri, ambapo mara nyingi kutelekezwa na kutengwa ni sababu kuu za wasiwasi wa kiuchumi.

Kulimbikiza mali nyingi huua furaha. Kunatuacha kwenye mtego wa wivu. Furaha iko kwingineko: kwa kuchagua mfumo rahisi wa maisha, kufanya kazi si kwa faida tu bali kutoa maana ya maisha, kushirikishana na wengine, kila mmoja anaweza saidia kujenga amani. Mungu atohi roho ya uwoga bali roho ya upendo na uwezo wa ndani.[18]

## MSAMAHA

Injili inatupa moyo wa kwenda mbali zaidi: haki lazima iongoze kwenye msamaha; jamii za binadamu haziwezi kuishi bila msamaha. Sehemu nyingi duniani, vidonda vya historia ni vya kina. Hivyo sote tuamue kumaliza ambavyo tunaweza kumaliza leo. Katika njia gani amani ya baadaye, inaandaliwayo katika moyo wa Mungu, yaweza kutumika kabisa.

Kuamini katika msamaha wa Mungu haimaanishi kusahau makosa. Ujumbe wa msamaha hauwezi kutumika kuruhusu ukosefu wa haki. La hasha, kuamini katika msamaha wa kunatuweka huru kutambua makosa yetu binafsi, vile vile makosa katika dunia inayotuzunguka. Ni juu yetu kurekebisha chochote ambacho kinaweza kufanywa vizuri. Katika njia hii ngumu tunapata msaada muhimu: katika kuunganika na Mungu katika Kanisa, Msamaha wa Mungu waweza kutolewa tena.

17 Bila shaka uhamiaji lazima urekebishwe, siyo kwa uwoga wa wageni bali kwa sababu za msingi za kuchanganyika kwao. Kwa wahamiaji, kupata malazi, kazi na kujifunza lugha ni vipaumbele. Kwa nchi mwenyeji, kutoa haki kunaenda sawa na matarajio halisi ya wajibu. Je, isiwe wito wa wakristu katika mazingira haya, kwa maisha yao, kuonyesha kuwa uwoga wa wageni hauwezi kuwa haki? Kuzoeana na kufahamiana vyaweza kuwa hatua ya kwanza katika kuushinda uwoga unaotokana na ujinga.

18 Angalia 2 Timotheo 1:7.

## Hatua zifuatazo katika Safari ya Imani Duniani

Pamoja na vijana kutoka ulaya yote, Bruda Alois pamoja na mabruda wengine watakwenda Moscow kuanzia Aprili 20-25, 2011, kusheherekea Juma kuu na Pasaka pamoja na Kanisa la Mashariki la Urusi.

Mkutano wa vijana wa 34 wa Ulaya utafanyika Berlin, Ujerumani, kuanzia Disemba 28, 2011 mpaka Januari 1, 2012.

Mkutano wa tatu wa kimataifa Afrika utafanyika Kigali, Rwanda kuanzia Novemba 14 hadi18, 2012.

Ujumbe uliopokelewa kwa ajili ya mkutano wa Rotterdam: www.taize.fr/sw

Kila binadamu anahitaji msamaha kama mkate wa kila siku.[19] Mungu anautoa kila siku daima, bila masharti, "Yule ambaye husamee dhambi zako zote."[20] Kufungua mikono ni tendo rahisi kuashiria kuwa tunatamani kuupokea.

Tunaposali Baba yetu: "Tusamehe makosa yetu, kama vile tunavyowasamehe...," samaha wa Mungu tayari unatugusa. Haya si maneno matupu: kunakitu kinatokea wakati tunasali tukitumia maneno ambayo Yesu alitufundisha. Na kisha tunakuwa tayari kusamehe na siyo kuhukumu haswa tunapokuwa tumetendewa makosa.

Kristu alitofautisha kati ya mtu na kosa lililotendwa. Mpaka pumzi yake ya mwisho msalabani, alikataa kumuhukumu yeyote. Na badala ya kupunguza kosa, alilichukua ndani mwake.

Kuna wakati ambapo tunashindwa kusamehe. Kidonda ni kikubwa sana. Tunahitaji kukumbuka kuwa msamaha wa Mungu haushindwi kamwe. Kwetu, wakati mwingine ni kwa hatua ndipo tunafanikiwa. Hamu ya kusamehe tayari ni hatua ya kwanza, hata kama nitakuwa imegubikwa na uchungu.

Kwa kusamehe, Mungu anafanya zaidi ya kuondoa kosa. Anatupa maisha mapya katika urafiki naye, ambao unawashwa tena usiku na mchana na Roho mtatkatifu.

Kuukaribisha na kushirikishana msamaha wa Mungu ni njia ambayo Kristu ameshafungua. Tunasonga mbele kwenye njia hiyo japokuwa tuna mapungufu na vidonda vyetu. Kristu hatugeuzi kuwa watu ambao tayari tumeshafikia lengo.

Sisi ni maskini wa Injili; kuwa wakristu haimaanishi kujifanya kuwa ni wazuri zaidi ya wengine. Kwa urahisi kinachotutofautisha ni kuamua kuwa wa Kristu. Katika kufanya uamuzi huu tunataka kukubali kabisa na daima.[21]

Na tunaweza kufanya ufumbuzi huu: msamaha tulioupokea au kutoa unaongeza furaha. Kufahamu kuwa mtu amesamehewa pengine ni moja ya furaha ya ndani na viachavyo huru wa furaha. Ni chanzo cha amani ya ndani ambayo Kristu anatuambia sisi. Kuwa amani itatuongoza mbali zaidi; itawaka nje kwa ajili ya wengine na dunia.[22]

fr. Alois

19 Suzanne de Dietrich (1891-1981), mwana theolojia wa Kiprotestanti ambaye mwanzoni mwa Taizé, alimtia moyo/shime Bruda Roger na mabruda wa mwanzoni kutosita kuweka nadhiri zao kwenye jumuiya kwa maisha yao yote, aliadika : "Mkristu ni mtu anayeishi katika msamaha, ambaye anajua kuwa kila siku anavunja amri za Mungu, lakini anarudi kwa Mungu kila siku na ambaye anajua, kwa uhakika mkubwa kuwa Mungu atakuwa na neno la mwisho katika maisha yake. Kristu amechua uongozi wa maisha yake, anawajibika kwa maisha yake mble ya Baba yake. Hayuko peke yake katika mapigano yake; yule ambaye pekee alitoa maisha yake hatomtelekeza kamwe. Uhakika wake hautokani tuu na yale yaliyokwisha kuwapo, bali katika Mungu alivyo mwaminifu na upendo wa Mungu uliofunuliwa katika Yesu Kristu. Hii ndiyo sababu kuwa kuendelea kwake hakumfungi macho hata kushindwa kwake hakukatishi tamaa. Mara zote anaamka tena kwasababu yeye si mali yake; ila ni ya kila mmoja."

20 Zaburi 103:3. Zaburi yote hii ni wimbo wa msamaha wa Mungu. Na nabii Isaya, katika kipindi kigumu ya historia, alilikumbusha taifa kuwa Mungu husamee, anasema: "Nimeyafagilia mbali mkosa yenu kama wingu ..." (Isaya 44:22).

21 "Wakristu si tuu wa Yesu Kristu kama bila shaka ilivyo kuwa binadamu yote ni wa Yesu, ila kufanya hivyo kwa katika njia ambayo kazi Yesu Kristu anaiyoifanya katika dunia pia ni maana ya matendo yao, pigano la kwanza ambalo Yesu Kristu anapigana katika giza dhidi ya giza kwa nia ambayo ni kwa ajili yao." (Karl Barth, 1886-1968)

22 Seraphim of Sarov, monk wa Kirusi wa karne ya kumi na tisa (1759-1833), aliandika: "Pata amani ya ndani na maelfu wanaokuzunguka wataokolewa."